

Je, mtu mwenye kuonekana na afya nzuri, anaweza kuwa na virusi vya UKIMWI?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, mtu anayeonekana na afya nzuri anaweza kuwa na virusi vya UKIMWI. Katika hatua ya mwanzo baada ya kuambukizwa mtu anakuwa na virusi vya UKIMWI kwenye damu lakini haonyeshi dalili zozote za kuumwa. Hatua hii i ii inaweza kuchukua zaidi ya miaka kumi! Hii ni hatari sana, kwa sababu kama unajamii ana na mtu mwenye kuonekana na afya nzuri, lakini ndani ya mwili tayari anavyo virusi vya UKIMWI, anaweza kukuambukiza. Njia pekee ya kuwa na uhakika kama mtu ameambukizwa na VVU au la ni kwa njia ya kupima damu katika Vituo maalumu vya kupima au hosipitalini. Kwa hiyo, kujamii ana bila kujikinga kwa kutumia kondomu i inawezekana kuhatarisha maisha yako, hata kama mpenzi wako ni mtu mwenye kuonekana na afya nzuri.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25906>